


# KUPUNGUA KWA DEMOKRASIA, KUZIDI KWA VURUGU

**Kuzimwa kwa mtandao mwaka wa 2023**

**#KeepItOn**

#KeepItOn

Ifuatayo ni tafsiri ya muhtasari wa ripoti ya #KeepItOn inayohusu Kuzimwa kwa mtandao mwaka wa 2023 ambayo yapatikana kwa ukamilifu hapa https://www.accessnow.org/keepiton-2023-report .

Kampeni ya #KeepItOn yaunganisha na kupanga mashirika ya kimataifa na juhudi za kumaliza kuzimwa kwa mtandao. Kampeni hii ilizinduliwa kwa muungano wa karibu mashirika 70 mwaka wa 2016 hapo RightsCon, Silicon Valley. Uanachama wa muungano huo umeongezeka na kufikia idadi ya wanachama 334 kutoka nchi 106 ulimwenguni kote, kuanzia vyama vya watu binafsi, wapiganiaji haki za kibinadamu, na watetezi makundi mengineyo pamoja na vituo vya tafiti mbalimbali, vituo vya uchunguzi, pamoja na mashirika ya habari.

Ripoti hii ni chapisho la Access Now kwa niaba ya muungano wa #KeepItOn na imeandikwa na Zach Rosson, Felicia Antonio, and Carolyn Tackett wakishirikiana na kijopo cha Access Now.

Waandishi wapenda kuwashukuru Donna Wentworth, Angela Alarcon, Bridget Andere, Golda Benjamin, Raman Jit Singh Chima, Giulio Coppi, Marwa Fatfta, Osei Manu kagyah, Natalia Krapiva, Jaimee Kokonya, Namrata Maheshwari, Peter Micek, Kassem Mnejja, Wai Phyo Myint, Shruti Narayan, Laura O'Brien, Naro Omo-Osagie, Gaspar Pisanu, Prateek, Alexia Skok, Vakau, Aymen Zaghdoudi, na Anastasiya Zhyrmont kwa mchango wao.  Pia tungependa kushukuru Advocacy Assembly Shutdown Academy, Athan, Cloudflare, Digitally Right, Internet Outage Detection and Analysis (IODA), Kentik, Miaan Group, Myanmar Internet Project, Open Observatory of Network Interference (OONI), Software Freedom Law Centre India (SFLC.in), pamoja na wanachama wengine wa muungano wa #KeepItOn kwa mchango wao muhimu na mawazo ya kina, kuhakiki data pamoja na vyanzo na kuchangia ripoti kwa jumla. Makosa yoyote, habari za kinyume na hali ilivyo, au mapungufu yoyote ni yetu sisi, na tunakubali marekebisho yoyote kutoka kwenu.

Mipangilio na michoro yote yametayarishwa na Loren Giordano na Sage Cheng.

## Angalizo Kuhusu Data Yetu

Ripoti hii ya #KeepItOn yaangazia matukio ya kuzimwa kwa mtandao yaliyorekodiwa na Access Now na muungano wa #KeepItOn mwaka wa 2023. Wakati tukjitahidi kuwa na data yenye ukamilifu mkubwa, data yetu inategemea vipimo vya kitaalamu pamoja na mengine yanayotegemea maelezo kama ripoti za vituo vya habari tofauti na maelezo ya watu binafsi. Kikwazo kikubwa katika mfumo huu tunaoutumia ni kuwa huenda kukawa matukio ya kuzimwa kwa mtandao ambayo hayakurepotiwa, na idadi ya mara za kuzimwa mtandao zinaweza kutofautiana na habari au ripoti mpya itakapopatikana baada ya kuchapichwa toleo letu. Mwaka wa 2023, tulipata maalumati ya ziada ya mwaka uliopita, ambayo tuliyaongeza katika ripoti yetu tukiyajaza mapengo hayo na kuyarekodi mabadiliko hayo ambayo yanapatikana katika hifadhidata yetu ya STOP katika kiunganishi hiki: https://accessnow.org/keepiton-data. Data iliyopo hapa inajumuisha habari iliyothabibiti zaidi kufikia sasa hadi wakati tunapochapisha toleo hili.

Tembelea https://accessnow.org/keepiton-data-methodology ili kupata habari kamilifu zaidi kuhusu mfumo wetu tunaoutumia, maswali yanayoulizwa mara kwa mara, na kazi ambayo bado inaendelea.

**May 2024**


CC BY

# I. Kuzimwa Mtandao Mwaka wa 2023: Mtazamo Wa Ulimwengu Mzima

# Muhtasari wa Data ya 2023

**Kuzimwa Kwa Mtandao Mwaka Baada Ya Mwaka***


■ Jumla ya idadi ya kuzima
□ Jumla ya idadi ya kuzima, sio pamoja na India




* Nambari hizi zinaonyesha data ya hivi karibuni inayopatikana kama ya kuchapishwa kwa ripoti hii na ni pamoja na sasisho za jumla zilizochapishwa hapo awali kwa miaka iliyopita.

**Idadi ya nchi ambazo kulitokea kuzimwa kwa mtandao**

| 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 27 | 23 | 28 | 36 | 34 | 39 | 40 | 39 |



**India: 116**
**Myanmar: 37**
**Iran: 34**
**Palestine: 16 ****
**Ukraine: 8 ****
**Pakistan: 7**
**Iraq: 6**
**Azerbaijan: 5**
**Ethiopia: 4**
**Senegal: 4**

Bangladesh: 3
Russia: 3
Jordan: 3
Libya: 3
China: 2
Guinea: 2
Mauritania: 2
Oman: 2
Tanzania: 2
Turkmenistan: 2
Sudan: 2
Syria: 2
Türkiye: 2
Algeria: 1
Brazil: 1
Cuba: 1
Gabon: 1
Indonesia: 1
Kenya: 1
Lebanon: 1
Msumbiji: 1
Nepal: 1
Qatar: 1
Saudi Arabia: 1
Somaliland: 1
Suriname: 1
Umoja wa Falme za Kiarabu: 1
Uganda: 1
Venezuela: 1

** Kufungwa kwa shughuli za serikali kuliwekwa na wahusika nje ya Palestina na Ukraine.

## Vichochezi Vya Kuzimwa Mtandao Mwaka wa 2023

| Kuzimwa wakati wa migogoro | Maandamano | Mitihani | Uchaguzi |
|---|---|---|---|
| Kuzimwa mara **74** katika nchi **9** wakati wa migogoro | Kuzimwa mara **63** katika nchi **15** wakati wa maandamano | Kuzimwa mara **12** katika nchi **6** ili "kukinga udanganyifu kwenye mitihani" | Kuzimwa mara **5** katika nchi **5** wakati wa uchaguzi |
| 2023: **74** | 2023: **63** | 2023: **12** | 2023: **5** |
| 2022: **36** | 2022: **63** | 2022: **8** | 2022: **5** |
| 2021: **19** | 2021: **39** | 2021: **11** | 2021: **7** |
| 2020: **15** | 2020: **16** | 2020: **8** | 2020: **10** |
| 2019: **52** | 2019: **65** | 2019: **8** | 2019: **12** |
| 2018: **2** | 2018: **45** | 2018: **11** | 2018: **12** |
| 2017: **3** | 2017: **37** | 2017: **7** | 2017: **6** |
| 2016: **3** | 2016: **27** | 2016: **6** | 2016: **5** |

**Emerging trigger in 2023:**

**Kutokana na majanga ya asili**

**4** kuzima ndani Nchi **4** wakati wa majanga ya asili

# Mielekeo Ya Kuzimwa Mtandao Mwaka wa 2023

**1. Kuzimwa kwa mtandao kunaendelea kupa nguvu ukiukaji wa haki za kibinadamu na kusababisha vurugu**

| | |
|---|---|
| Kuzimwa kwa mtandao mara **51** katika nchi **11** kuhusiana na ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu uliosajiliwa *** | Azerbaijan, Ethiopia, Iran, Jordan, Mauritania, Myanmar, Palestine, Russia, Somaliland, Sudan, Ukraine |

*** Ukiukaji mkubwa wa haki za kibinadamu unahusisha hali za vurugu zilizoshuhudiwa zikijumuisha mauaji, kuteswa, ubakaji au uhalifu mwingine wa kivita unaotekelezwa na serikali, wanajeshi, na polisi au amrijeshi wengineo.

**2. Mamlaka lazime wajizuie kurasimisha kuzimwa kwa majukwaa ya kijamii**

Kuzimwa mara **53** katika nchi **25** countries in 2023, ikiwa ongezeko kutoka kuzimwa mara **39** katika nchi **29** 2022

| | |
|---|---|
| Grindr ni jukwaa la kijamii la pili lililozuiwa zaidi katika majukwaa ya mtandao nje ya nje na India, baada ya Facebook, iliyoathiri watu katika nchi **12** na iliyolenga nafasi za LGBTQ+ | China, Indonesia, Iran, Jordan, Lebanon, Oman, Pakistan, Qatar, Saudi Arabia, Tanzania, Türkiye, United Arab Emirates |

## 3. Watekelezaji sugu wamekita na kujizatiti katika kutumia ufungaji wa mtandao

**Siku 1,153** tangu Nov. 4, 2020
Tigray, Ethiopia

**Siku 864** tangu Aug. 2021 ****
Dazeni ya miji nchini Myanmar

**Siku 694** tangu Feb. 2022
Panjgur, Pakistan

**Tukio za kuzimwa**
**35**
**shutdowns ziliendelea toka 2023 kuingia 2024**
Watu katika nchi **17** walikumbwa na ufungaji wa mtandao **mwaka mzima** 2023

****Idadi ya siku toka Dec. 31, 2023

## 4. Upeo wa Maeneo yanayofunga Mtandao yanazidi kupanuka

Mwaka wa 2023, **30.4%** wa ufungaji wa mtandao ulikuwa wa kiwango kidogo (ukidhuru mji, kata au kijiji kimoja), kwa upande mwingine mwaka wa 2022 ulipata ufungaji wa kiwango hiki **46.8%**.

Matukio **80** ya kuzimwa kwa mtandao yaliathirisehemu zaidi ya moja au nchi nzima, ambayo ndiyo idadi kubwa iliyowahi kusajiliwa tangu 2016.

| Tangu 2016 | Watekelezaji wapya 2023 |
|---|---|
| **1,458**<br>Ufungaji wa mtandao kote duniani | **Kenya *******<br>**Mozambique**<br>**Nepal**<br>**Suriname**<br>***** Kuzimwa kwa mara ya kwanza kwa idhini ya serikali ya Kenya; Kuzimwa kwa 2020 kulisababishwa na watu wengine |
| **82**<br>Nchi zilizoadhirika<br><br>**334**<br>Wanachama wa #KeepItOn kutoka nchi **106** | **Lebanon**<br>**Qatar**<br>**Umoja wa Falme za Kiarabu**<br>Nchi zilizo na uzuizi wa jukwaa mbalimbali kwa zaidi ya mwaka mmoja zinasajiliwa kwenye hifadhidata ya STOP kwa mara ya kwanza |

## Muhtasari wa Mkoa Afrika mnamo 2023

| 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|
| kuzimwa mara 19 | kuzimwa mara 9 | kuzimwa mara 17 |
| nchini 12 | nchini 7 | nchini 9 |

**Ethiopia:** 4
**Senegal:** 4

**Guinea:** 2 **Tanzania:** 2
**Gabon:** 1 **Somaliland:** 1 **Uganda:** 1

**Watekelezaji wa mara ya kwanza:**

**Kenya:** 1
**Msumbiji:** 1

| | |
|---|---|
| 2022 | 44.5% |
| 2023 | 58.8% |

**58.8% ya kuzimwa mtandao kulihusiana na maandamano**

Senegal: 4 Ethiopia: 2 Gabon: 1 Guinea: 1 Msumbiji: 1 Somaliland: 1

| | |
|---|---|
| 2022 | 33.3% |
| 2023 | 58.8% |

**58.8% ya kuzimwa mtandao kulilenga majukwaa ya mtandao**

Ethiopia: 2 Guinea: 2 Senegal: 2 Tanzania: 2 Kenya: 1 Uganda: 1

** Tazama sehemu ya Mashariki Ya kati na Afrika Ya Kusini (MENA), katika ripoti kamili iliyo na habari kuhusu kuzimwa kwa mtandao Algeria, Libya, Mauritania, na Sudani.

Mwaka wa 2023, tuliona kuzuka tena kwa ufungaji wa mtandao Afrika ambapo matukio 17 yalirekodiwa katika nchi **tisa** - takriban maradufu ya mara **tisa** ya kuzimwa kwa mtandao katika nchi **saba** mwaka wa 2022— ambao ndiyo idadi ndogo zaidi katika eneo hili ambalo lilikuwa na hali ya kupungua kwa matukio ya kufunga mtandao tangu mwaka wa 2020. Ongezeko hili la ghafla la mwaka wa 2023 linatia wasiwasi kukhusu kutumika kufunga mtandao kama silaha katika eneo hili.

Mbali na kuwa haki za kibinadamu zazidi kudorora barani Afrika,[1] serikali nyingi zimefunga mitandao nyakati za maandamano, uchaguzi, mitihani ya kimataifa, na kwenye vurugu. Lengo : **Kunyamazisha sauti zinazopingana na serikali na kukwamisha kuenea na kueneza habari bila pingamizi.**

Baada ya nchi saba, kwa mshangao mkubwa, kufunga mtandao kwa mara ya kwanza mwaka wa 2021, mwaka wa 2022 kulipatikana afueni, kwa kutojitikeza nchi mpya zilizoingia katika orodha hii ya wahalifu. La kusikitisha, watekelezaji wapya wawili walizuka mwaka wa 2023: Msumbiji, ilitatiza mtandaowa simu za rununu wakati serikali ikikabiliana vikali na maandamano kuhusu uchaguzi,[2] na Kenya iliziba mtandao wa Telegram wakqati wa mitihani ya kimataifa,[3] wakienda kinyume na msimamo wa kutofunga mitandao ya

1 Freedom House (2024). *NEW REPORT: Africa Marks a Decade of Decline in Freedom, with 2023 Being Marred by Electoral Violence and Civil Conflict.* https://freedomhouse.org/article/new-report-africa-marks-decade-decline-freedom-2023-being-marred-electoral-violence-and/

2 Club of Mozambique (2023). *CIP Mozambique Elections: Internet cut, counting starts.* https://clubofmozambique.com/news/cip-mozambique-elections-internet-cut-counting-starts-246517/

3 Access Now (2023). *Open letter: clarification on Telegram blocking in Kenya.* https://www.accessnow.org/press-release/open-letter-clarification-on-telegram-blocking-in-kenya/

kijamii waliouchukua mwaka mmoja nyuma wakati wa uchaguzi.[4]

Mbali na changamoto hizi zote, kulikuwa na hali za kusherehekea mwaka wa 2023. Uongozi wa Jamhuri Ya Kidemokrasia Ya Kongo (DRC), Nigeria, na Sierra Leone, waliahidi na wakatekeleza kauli ya kutofunga mtandao wakati wote wa uchaguzi - jambo la muhimu sana, kwa sababu ya athari mbaya ya kuzimwa kwa mtandao kunavyoathiri demokrasia.[5]

Tulishuhudia pia harakati za kutia moyo katika vita vya kisheria dhidi ya kuzimwa kwa mtandao barani Afrika Mwaka wa 2023, Mahakama ya Jumuiya ya Kiuchumi ya Mataifa Ya Afrika Magharibi (ECOWAS), iliendelea kuipa nguvu sheria na kutilia mkazo kutofunga mtandao, katika maamuzi dhidi ya kuzimwa kwa mtandao huko Guinea, kuwa ni kinyume cha sheria.[6]

## Kuzimwa kwa Mtandao Wakati Wa Maandamano, vurugu la kisiasa na ukosevu wa utulivu

Bara Afrika lilikumbwa na maandamano yaliyotapakaa kote yaliyoandaliwa kupinga hali ngumu za kiuchumi, kudorora kwa mihimili ya kidemokrasia, na ukosevu wa utulivu wa kisiasa mwaka wa 2023. Ili kukabiliana na hali hizi, mamlaka yalichukua hatua ya kufunga mtandao mara **10** - kufanya maandamano yaongoze kama kichochezi kikuu kilichosababisha mtandao kuzimwa Afrika kwa wa **tatu** mfululizo.

Kwa ajili ya kukumbwa na maandamano ya mara kwa mara, pamoja na kusuasua kwa kisiasa, mamlaka ya Senegal yalitatiza mtandao na kupatikanwa kwake, au hata kuzuia majukwaa ya kijamii kabisa, mara **nne**. Baada ya maandamano kuzuka Dakar na Ziguinchor, Juni 1, kufuatia kushikwa kwa kiongozi wa upinzani Ousmane Sonko, mamlaka ilifunga mtandao wa majukwaa yote ya kijamii ikiwemo WhatsApp, Telegram, Instagram, X (awali Twitter), na YouTube.[7] Siku tatu baadaye, mamlaka ilijumuisha mtandao wa simu za rununu.[8]

Sonko aliwahi kushikwa tena Julai 28, 2023. Maandamano yalipozuka tena kupinga kushikwa kwake, mamlaka yalitapia kuzima mtandao na kuzuia TikTok.[9] Ingawa mamlaka yalifungua mtandao wa simu za rununu tarehe 5 Agosti, Tiktok iliendelea kufungiwa bila maelezo yoyote hadil Februari 2024.[10]

Serikali ya Senegali ilijaribu kuhalalisha kitendo chake cha kufunga mtandao kama hatua muhimu ya kuzuia kuenea arafa za kueneza chuki na za uhaini, huku serikali ikilaumu mitandao ya kijamii kwa kuchochea maandamano hayo.[11] Serikali ilikuwa awali imefunga mtandao ili kukomesha maandamano baada ya Sonko kufungwa jela mwaka wa 2021.[12] insi hii ya kujirudiarudia ya kuzima mtandao ili kuwanyamazisha wapinzani wa kisiasa, pamoja na kushikwa kwa wanahabari, na msukumo wa Rais Macky Sall wa kutaka kuweka sheria ya ya kudhibiti na kutoruhusu mitandao ya kijamii, ni dalili moja ya uasi unaopelekea

4 Access Now (2023). *Warning: blocking online platforms in Kenya will spread election disinformation.* https://www.accessnow.org/press-release/kenya-online-platforms-social-media-blocking-internet-shutdown-election/

5 Access Now (2023). *2023 elections and internet shutdowns watch.* https://www.accessnow.org/campaign/2023-elections-and-internet-shutdowns-watch/; Actu7 (2023). *Elections 2023: "On ne coupera pas la connexion internet le jour du vote" (Peter Kazadi).* https://actu7.cd/2023/12/19/elections-2023-on-ne-coupera-pas-la-connexion-internet-le-jour-du-vote-peter-kazadi/; Sahara Reporters (2023). *Nigerian Communications Commission Says No Network Shutdown During General Elections.* https://saharareporters.com/2023/02/24/nigerian-communications-commission-says-no-network-shutdown-during-general-elections/; Felicia Anthonio (@FelAnthonio). X post. 4:50 pm. June 29, 2023. https://x.com/FelAnthonio/status/1674460297715757080

6 Media Defence (2023). *ECOWAS Court condemns internet shutdown in Guinea.* https://www.mediadefence.org/news/ecowas-court-condemns-internet-shutdown-in-guinea/

7 Technext (2023). *Senegal limits social media access following protests over sentencing of opposition leader.* https://technext24.com/2023/06/03/sonko-senegal-social-media/

8 Reuters (2023). *Senegal government cuts mobile internet access amid deadly rioting.* https://www.reuters.com/world/africa/senegal-government-cuts-mobile-internet-access-amid-deadly-rioting-2023-06-04/

9 Reuters (2023). *Senegal blocks TikTok in widening clampdown on dissent.* https://www.reuters.com/world/africa/senegal-suspends-tiktok-saying-it-was-threatening-stability-2023-08-02/

10 Access Now (2023). *Stop the internet shutdowns: Senegal authorities must end censorship.* https://www.accessnow.org/press-release/internet-shutdowns-senegal/; Africanews (2023). *Senegal declines to lift TikTok ban.* https://www.africanews.com/2023/10/06/senegal-declines-to-lift-tiktok-ban/

11 News24 (2023). *Senegal shuts down internet as riots erupt after opposition leader sentenced for sex crime.* https://www.news24.com/news24/africa/news/senegal-shuts-down-internet-as-riots-erupt-after-opposition-leader-sentenced-for-sex-crime-20230602/

12 Bloomberg (2021). *Senegal Shuts Down TV Stations, Internet Disrupted Amid Protests.* https://www.bloomberg.com/news/articles/2021-03-05/senegal-shuts-down-tv-stations-internet-disrupted-amid-protests/

nidhamu ya udikteta wa kidijitali.[13] Tunapoangazia uongozi upya baada ya uchaguzi wa February na Machi 2024uliokumbwa na migogoro kadha wa kadha, tunatumai uongozi wa Senegal uta-#KeepItOn.[14]

Hali ya uhuru wa wanahabari na haki za kibianadamu nchini **Guinea** umedorora kwa kiasi kikubwa tangu wanajeshi kuipendua serikali ya Alpha Konde mwaka wa 2021.[15] Mei 2023, wanajeshi walijibu matakwa na malalamishi ya asasi za kiraia zikitia wito wa maandamano dhidi ya junta, kwa kufunga WhatsApp, Facebook, Facebook Messenger, Telegram, Snapchat na Instagram kwa miezi kadhaa.[16] Ingawa Jeshi lilikataa kuwajibika kwa kuzima mtandao na kuhusisha hitilafu za kimitambo kama sababu iliyosababisha tatizo hilo,[17] ushahidi uliokusanywa na Open Observatory of Network Inteference(OONI), unaashiria kuwa kuzimwa kwa mtandao kulipitia TLS ambako ni kwa makusudi.[18] Jeshi lilizidi kuikandamiza hali kwa kuendeleza kuzimwa kwa mtandao mwezi wa Novemba, ikakwamisha ishara za redio, vituo vya TV, na kufunga mitandao ya kijamii,[19] mtandao mwishowe ulipata kufunguliwa Februari 22, 2024.[20]

**Ethiopia**, ambako mizozo na vurugu bado yanaendelea, na maeneo ya Tigray yamefungiwa mtandao kwa miaka, mamlaka inazidi kutumia kufunga mtandao kama silaha ya kukabiliana na ukosefu wa amani na utulivu nchini. Februari 4, 2023, baada ya viongozi wa makanisa kuitisha maandamano, serikali ilizuia mitandao ya kijamii ikiwemo Facebook, TikTok na Telegram na wakaendeleza kuzimwa huko kwa miezi mitano.[21] Mamlaka ya Ethiopia iliamuru maandamano hayo yakomeshwe kwa kuwa yalikuwa kinyume na sheria, na kuwashauri raia wasishiriki ili wasizushe vurugu.[22]

Mwisho, **Mauritania**, serikali ilifunga mtandao Machi 6, 2023, punde tu baada ya wafungwa wanne waliotangazwa na Wizara Ya Mambo Ya Ndani kuwa ni magaidi, kutoweka toka jela huko Nouakchott.[23] Watu walishindwa kuunganishwa mtandaoni wakati ambapo serikali ilikuwa ikifanya uchunguzi wa nchi nzima kuwatafuta wahabusu hao, hali iliyohatarisha maisha yao.[24] Hii ilikuwa moja ya mara kadhaa ambapo mtandao ulifungwa kwa sababu ya kukimbia mahabusu jela ulimwenguni mwaka wa 2023 - swala jipya lililoibuka la kusingizia kuzimwa kwa mtandao, kijisababu kilichotumiwa vibaya na serikali na vyombo vya usalama.

## Kuzimwa kwa Mtandao Nyakati za Uchaguzi

Baada ya mwaka wa uchaguzi wa utulivu kwa kanda hiyo mnamo 2022, Access Now iliweka nchi **11** za Afrika

**13** The Africa Report (2021). *Senegal's president joins the chorus against Twitter and Facebook.* https://www.theafricareport.com/99491/senegals-president-joins-the-chorus-against-twitter-and-facebook/; Media Foundation for West Africa (2024). *Senegal: Six journalists arrested over Minister's defamation complaint.* https://www.mfwa.org/issues-in-focus/senegal-six-journalists-arrested-over-ministers-defamation-complaint/

**14** Al Jazeera (2024). *Senegal's top court confirms Bassirou Diomaye Faye's election victory.* https://www.aljazeera.com/news/2024/3/29/senegals-top-court-confirms-bassirou-diomaye-fayes-election-victory/

**15** Reporters Without Borders (2023). *Unprecedented press freedom violations by Guinea military junta.* https://rsf.org/en/unprecedented-press-freedom-violations-guinea-s-military-junta/

**16** Access Now (2023). *Stop shutting down the internet in Guinea: authorities must #KeepItOn amidst protest.* https://www.accessnow.org/press-release/stop-shutting-down-the-internet-guinea/

**17** Guinéenews (2023). *Perturbation de la connexion internet en Guinée: quand Ousmane Gaoual fait le faux-fuyant.* https://guineenews.org/perturbation-de-la-connexion-internet-en-guinee-quand-ousmane-gaoual-fait-le-faux-fuyant/

**18** Open Observatory of Network Interference (@OpenObservatory). X post. 10:18 am. May 22, 2023. https://x.com/OpenObservatory/status/1660591036316499968; *see also* Access Now (2022). *A taxonomy of internet shutdowns: the technologies behind network interference.* https://www.accessnow.org/shutdown-taxonomy-report

**19** Media Foundation for West Africa (2023). *Radio airwaves jammed, social media blocked in Guinea.* https://www.mfwa.org/issues-in-focus/radio-airwaves-jammed-social-media-blocked-in-guinea/

**20** Open Observatory of Network Interference (@OpenObservatory). X post. 3:23 pm. February 23, 2024. https://x.com/OpenObservatory/status/1761049064752177282/

**21** Access Now (2023). *Ethiopia authorities must stop blocking social media.* https://www.accessnow.org/press-release/ethiopia-social-media-protest/

**22** Addis Standard (2023). *News: Joint Security, Intelligence Task Force cautions against unauthorized rallies, threatens to take actions as Orthodox Church Schism takes toll.* https://addisstandard.com/news-joint-security-intelligence-task-force-cautions-against-unauthorized-rallies-threatens-to-take-action-calls-as-orthodox-church-schism-takes-toll/

**23** Cloudflare Radar (@CloudflareRadar). X post. 8:19 am. March 6, 2023. https://x.com/CloudflareRadar/status/1632747652608581633/

**24** Reuters (2023). *Two guards killed in gunfire as four break out of jail.* https://www.reuters.com/world/africa/two-guards-killed-gunfire-four-break-out-mauritania-jail-2023-03-06/

ambazo hapo awali ziliweka vizuizi vya mtandao kwenye darubini ya #KeepItOn Election Watch ya 2023 - Benin, DRC, Eswatini, Gabon, Liberia, Nigeria, Sierra Leone, na Zimbabwe.[25]

Miongoni mwa nchi zilizo kwenye orodha ya uangalizi, ni Gabon pekee iliyotekeleza ufungaji wa mtandao, lakini kama tulivyoona, Msumbiji ikawa mkosaji kwa mara ya kwanza wakati wa uchaguzi wa serikali za mitaa. Uganda iliendelea kuzuia Facebook, kama ilivyokuwa tangu uchaguzi wa 2021, na kufanya idadi ya kuzimwa kwa mtandao kwa ajili ya uchaguzi barani Afrika kuwa **tatu**.

Serikali ya Ali Bongo nchini **Gabon**, ambayo awali imeweka vizuizi wakati wa uchaguzi uliopita, ilizuia upatikanaji wa mtandao na kuweka amri ya kutotoka nje usiku baada ya uchaguzi kuzimwa Agosti 26, huku kukiwa na ripoti za ukandamizaji wa wapiga kura na utovu wa nidhamu katika vituo mbalimbali vya kupigia kura.[26] Ukosefu wa waangalizi wa uchaguzi wa kimataifa na kusimamishwa kwa matangazo ya kigeni kabla ya uchaguzi tayari ulikuwa umetia shaka juu ya uwazi na haki ya uchaguzi.[27] Kisichoshangaza, Kituo cha Uchaguzi cha Gabon yaani Gabonese Election Centre kilitangaza Bongo kuwa mshindi, tangazo ambalo lingeongeza muda wake wa urais katika muhula wa tatu.[28] Hata hivyo, jeshi lilifanya mapinduzi, kufuta matokeo ya uchaguzi, na mara moja kurejesha upatikanaji wa mtandao, na kumaliza kuzimwa mtandao kwa siku tatu.[29]

Nchini **Msumbiji**, mamlaka zilijibu sauti pinzani wakati wa uchaguzi wa serikali za mitaa mwezi Oktoba kwa kuwakandamiza wanachama wa upinzani, waandishi wa habari, na watetezi wa haki za binadamu, ikiwa ni pamoja na kukamatwa kiholela na kupigwa risasi.[30] Kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi kulizusha maandamano makubwa kote nchini dhidi ya madai ya wizi wa kura,[31] na hapo ndipo, kwa mara ya kwanza katika rekodi zetu, mamlaka zilivuruga upatikanaji wa mtandao, na kuufunga kwa takriban masaa matatu huku kukiwa na ripoti za kukatika kwa umeme.[32]

Uvurugaji huu unawakilisha mashambulizi mabaya dhidi ya demokrasia. Lakini kama tulivyoonyesha awali, DRC, Nigeria, na Sierra Leone, wote awali watekelezaji wa wa ufungaji wa mtandao, kila mmoja alifanya na kutekeleza ahadi za kuhakikisha watu wana uwezo wa kuwasiliana wakati wa uchaguzi.[33] Nchi za Afrika kwa hivyo ziliongoza njia duniani kote kati ya watekelezaji wa zamani katika kuonyesha kujitolea kwa mageuzi, mfano mzuri kwa nchi katika kanda na duniani kote. Kulikuwa na habari njema zaidi mwezi Machi 2024, wakati Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Haki Za Watu yaani African Commission on Human and Peoples' Rights (ACHPR) ilipotoa azimio lake la kulaani kuzimwa kwa mtandao wakati wa uchaguzi barani Afrika, kwa kutambua umuhimu wa upatikanaji wa mtandao kwa ajili ya kutambua haki za binadamu, na kutoa wito kwa mataifa kuchukua hatua za kuhifadhi mawasiliano wakati wa uchaguzi, ikiwa ni pamoja na kupitishwa sheria muafaka na hatua nyingine.[34]

25 *Supra* note 5. Access Now (2023).

26 Reuters (2023). *Gabon cuts internet, imposes curfew amid election voting delays.* https://www.reuters.com/world/africa/gabon-vote-president-bongo-seeks-extend-56-year-family-dynasty-2023-08-26/

27 *Ibid*.

28 Reuters (2023). *Gabon President Ali Bongo wins third term after disputed election.* https://www.reuters.com/world/africa/gabon-president-ali-bongo-wins-third-term-after-disputed-election-2023-08-30/

29 Reporters Without Borders (2024). *Reacting to Gabonese army's post-coup statements, RSF issues ten recommendations for respecting press freedom.* https://rsf.org/en/reacting-gabonese-army-s-post-coup-statements-rsf-issues-ten-recommendations-respecting-press/

30 Club of Mozambique (2023). *Mozambique: Shootings, arrests, internet and power outages taints vote counts, Sala da Paz says.* https://clubofmozambique.com/news/mozambique-shootings-arrests-internet-and-power-outages-taint-vote-counts-sala-da-paz-says-246532/

31 ISS Africa (2023). *Fraudulent municipal elections cripple democracy in Mozambique.* https://issafrica.org/iss-today/fraudulent-municipal-elections-cripple-democracy-in-mozambique/

32 allAfrica (2023). *Mozambique: Internet Shutdown as Polls Close.* https://allafrica.com/stories/202310120129.html/

33 *Supra* note 5.

34 African Commission on Human and Peoples' Rights (2024). *Resolution on Internet Shutdowns and Elections in Africa - ACHPR. Res.580 (LXXVIII)2024.* https://achpr.au.int/index.php/en/adopted-resolutions/580-internet-shutdowns-elections-africa-achprres580-lxxvii/

## // Kuzimwa kwa Mtandao Nyakati Za Migogoro : Ethiopia

Matumizi ya serikali ya Ethiopia ya uzimaji wa mtandao ni hatari hasa wakati wa vita. Hata hivyo licha ya malalamiko ya umma, mamlaka zinaendelea kuwaweka watu katika kiza cha mawasiliano na maisha yao kuwa hatarini.

Mnamo Aprili 2023, baada ya jeshi la Ethiopia kuhamia kunyang'anya silaha Vikosi Maalum vya Amhara (Amhara Special Forces) na washirika wengine wa kikanda, maandamano na vurugu zilizuka katika miji ya Gondar, Kobo, Sekota, Weldiya, na miji mingine katika mkoa wa Amhara. Wakati hali ikizidi kuwa mbaya, mamlaka zilizuia upatikanaji wa mtandao wa simu katika eneo la Amhara, na kuwakatiza mamilioni ya watu kutoka maeneo mengine ya dunia.[35] Wakati mapigano yalipoongezeka mwezi Agosti, serikali ilitangaza hali ya dharura na kwa mara nyingine tena kufunga huduma za intaneti, huku kukiwa na taarifa za kuchafuka kwa utakaso wa kikabila.[36] Mamlaka pia iiliwakamata waandishi wa habari na kuzuia upatikanaji wa vyombo vya habari katika msako dhidi ya kuripoti kwa migogoro iliyokuwa inaendelea.[37]

Matumizi taratibu ya Ethiopia ya kufunga mtandao na kudhibiti vyombo vya habari wakati wa vita hufanya kuwa vigumu sana kwa watu kupata habari za kuokoa maisha, pamoja na kupata msaada wa kibinadamu, ikiwa ni pamoja na huduma za dharura za afya, maji, chakula, makazi, na huduma za ulinzi.[38] Uvurugaji pia hufanya iwe vigumu kuthibitisha na kuandika kiwango na upeo wa ukatili unaofanywa na pande zinazopigana. Tume ya Haki za Binadamu ya Ethiopia imeripoti matukio ya mauaji ya kiholela, unyanyasaji wa kijinsia, unyanyasaji wa kimwili, ukimbizi, na uharibifu wa mali ya raia na vikosi vya usalama vya serikali na wanamgambo wa serikali, pamoja na hali mbaya inayoashiria kuongezeka kwa ukatili, ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa unyanyasaji wa kijinsia.[39] Baada ya zaidi ya mwaka mmoja wa mapigano wakati wa kuchapishwa, vita na mashambulizi dhidi ya raia yanaendelea kuongezeka.[40] Baada ya zaidi ya mwaka mmoja wa mapigano wakati wa kuchapishwa, vita na mashambulizi dhidi ya raia yanaendelea kuongezeka. Maafa haya, ambayo yanaweza kuwa uhalifu wa kivita, ni ukiukaji mkubwa wa sheria za kimataifa za kibinadamu.[41]

Hata baada ya mgogoro kumalizika, kuzimwa kwa mtandao huzidisha maumivu na mateso na kuzuia kupona kutokana na vurugu na uharibifu. Tunapoandika, mchakato wa amani ulioanzishwa mnamo Novemba 2022 kufuatia mgogoro wa miaka mingi na mgogoro wa kibinadamu huko Tigray bado haujafaulu.[42] Kuna ukosefu wa usalama unaoendelea, ukame, njaa, na kukatiizwa mara kwa mara kwa misaada ya kibinadamu, ambayo yote yanaendelea kuwadhuru raia wanaojaribu kurudisha maisha yao pamoja baada ya vita.[43] Mashambulizi yasiyo na huruma kwenye miundombinu ya mawasiliano ya simu ambayo tayari ni dhaifu, na hali ya kujikokota ya mamlaka kukarabati na kurekebisha miundombinu hii, yamewaacha watu wengi huko Tigray ama wamekatizwa kabisa kutoka mawasiliano, na kulazimishwa kusafiri nje ya jamii yao kupata mawasiliano, au wapate huduma ya polepole sana na isiyotegemeka. Kama tulivyoonyesha, inamaanisha kuwa kufikia mwisho wa 2023, wengi walikuwa wametimia siku 1,153 za kukatizwa, wakati walipohitajia msaada zaidi.

35 The Guardian (2023). *Gun battles erupt in Ethiopia as PM axes Amhara region's security force.* https://www.theguardian.com/global-development/2023/apr/12/gun-battles-erupt-in-ethiopia-as-pm-axes-amhara-regions-security-force/

36 The Guardian (2023). *Ethiopia declares a state of emergency in Amhara amid increasing violence.* https://www.theguardian.com/global-development/2023/aug/04/ethiopia-declares-a-state-of-emergency-in-amhara-amid-increasing-violence/; OHCHR (2023). *Comprehensive investigative findings and legal determinations. International Commission of Human Rights Experts on Ethiopia.* https://www.ohchr.org/sites/default/files/documents/hrbodies/hrcouncil/chreetiopia/a-hrc-54-crp-3.pdf

37 Addis Standard (2023). *News: CPJ urges authorities to release journalist detained without charge.* https://addisstandard.com/news-cpj-urges-authorities-to-release-journalist-detained-without-charge/

38 *See supra* note 36.

39 Ethiopian Human Rights Commission (2023). *Amhara Region: Concerning human rights violations in the context of the armed conflict.* https://ehrc.org/amhara-region-concerning-human-rights-violations-in-the-context-of-the-armed-conflict/

40 Foreign Policy (2024). *Ethiopia's Amhara Conflict Could Spark Civil War.* https://foreignpolicy.com/2024/03/06/ethiopia-amhara-conflict-civil-war/

41 Amnesty International (2024). *Ethiopia: End extrajudicial Executions in Amhara region, bring perpetrators to justice.* https://www.amnesty.org/en/latest/news/2024/02/ethiopia-end-extrajudicial-executions-in-amhara-region-bring-perpetrators-to-justice/

42 Access Now (2022). *After years in the dark, Tigray is slowly coming back online.* https://www.accessnow.org/tigray-shutdown-slowly-coming-back-online/

43 *See* AP News (2024). *Ethiopia's Tigray region is now peaceful, but extreme hunger afflicts its children.* https://apnews.com/article/ethiopia-hunger-crisis-tigray-malnutrition-health-7e085f5bd2ac138a27fdc0ec544fb296/

## Kufungwa kwa Mitandao ya Kijamii

Katika 10 kati ya matukio 17 ya bara la Afrika ya kuzimwa kwa mtandao, mamlaka yalilenga mitandao ya kijamii. Wakati wa maandamano nchini Ethiopia na Senegal na uchaguzi nchini Guinea, serikali zilizuia upatikanaji wa mitandao ya kijamii, katika juhudi za kuzuia mtiririko wa habari na kukandamiza upinzani. Mamlaka nchini Kenya zilizuia upatikanaji wa Telegram kwa mara ya kwanza wakati wa mitihani ya kitaifa mwezi Novemba.[44] Wlwapo serikali haikutoa amri yoyote rasmi ya kufungwa kwa mtandao , kizuizi hicho kiliripotiwa kuwekwa ili kuzuia kuenea maswali ya mitihani ilivyovuja.[45]

Hatua ya Uganda kuzuia Facebook kuanzia wakati wa uchaguzi wa 2021 imeendelea kusababisha uharibifu mkubwa wa haki za binadamu na soko la kidijitali.[46] Hata baada ya vitisho vya kisheria kutoka kwa Kampuni ya Urban Smart Traders Business Association Limited mnamo Oktoba 2023, na pingamizi inayoendelea iliyofunguliwa katika Mahakama ya Afrika Mashariki mwaka 2021, serikali pia haijaondoa kizuizi hicho.[47] Mnamo Januari 2024, Waziri wa TEHAMA na Mwongozo wa Kitaifa wa Uganda alidai kuwa Tume ya Mawasiliano ya Uganda (UCC) ilikuwa katika mazungumzo na Facebook juu ya jinsi ya kuanza tena kufanya kazi nchini baada ya kizuizi cha miaka mitatu, lakini tunapoandika, matokeo ya mazungumzo hayo bado hayajawa na uhakika.[48]

Nchini Tanzania, mamlaka ziliweka vizuizi vya huduma za mtandao kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2020, ikiashiria kuongezeka msimamo mkali wa serikali dhidi ya huduma za kidijitali. Mnamo Januari, mamlaka zilizuia ufikiaji wa Grindr, kama sehemu ya kampeni pana ya kukandamiza haki za watu wa LGBTQ + na jamii husika.[49] Mnamo Agosti, pia walizuia Clubhouse, mtandao wa kijamii ambao ni wa gumzo la sauti, bila maelezo.[50] Miezi michache baadaye, Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilitoa maagizo ya kuzuia matumizi ya mitandao ya kibinafsi (VPNs), ambayo inaweza kusaidia watu kupata tena fursa ya majukwaa yaliyozuiwa.[51]

---

44 Access Now (2023). *Telegram in Kenya: keep people connected during national exams.* https://www.accessnow.org/press-release/telegram-kenya-connected-national-exams/

45 TechCabal (2023). *Telegram is disrupted in Kenya as internet authorities remain silent.* https://techcabal.com/2023/11/21/telegram-offline-in-kenya/

46 Monitor (2022). *We'll reopen Facebook when they stop playing games – Museveni.* https://www.monitor.co.ug/uganda/news/national/we-ll-reopen-facebook-when-they-stop-playing-games-museveni-4064942


47 allAfrica (2023). *Uganda: Govt Given Two Week Ultimatum to Reopen Facebook or Face Legal Action.* https://allafrica.com/stories/202310250583.html; East African Court of Justice (2021). *Reference No. 12 of 2021 East African Law Society v. The Attorney General of the Republic of Uganda & The Secretary General of the East African Community.* https://www.eacj.org/?cases=reference-no-12-of-2021-east-african-law-society-v-the-attorney-general-of-the-republic-of-uganda-the-secretary-general-of-the-east-african-community

48 New Vision (2024). *Govt, Facebook in talks to end three year blockade.* https://www.newvision.co.ug/category/news/govt-facebook-in-talks-to-end-three-year-bloc-NV_179442/

49 OONI (2023). *Tanzania blocked Grindr*. https://explorer.ooni.org/findings/203466718601/

50 OONI (2023). *Tanzania blocked Clubhouse.* https://explorer.ooni.org/findings/185407756401/

51 CIO Africa (2023). *Tanzania Imposes Ban On VPN Usage Without A Permit.* https://cioafrica.co/tanzania-imposes-ban-on-vpn-usage-without-a-permit/




#KeepItOn

# KUPUNGUA KWA DEMOKRASIA, KUZIDI KWA VURUGU

## Kuzimwa kwa mtandao mwaka wa 2023

CC BY